



Wanawake waungana kukausha samaki kwa

Kushirikiana kuleta maendeleo

Ule msemu wa 'umoja ni nguvu, utengano ni dhaifu' unaweza kuwa wa zamani lakini bado una maana kwa Kikundi cha Kuchakata Samaki cha Yehowa Enye Kplorlanye cha huko Dzemeni, katika Mkoa wa Volta nchini Ghana. Hapo mwanzo kila mmoja alifanya kazi hiyo peke yake, lakini sasa wanashirikiana kama kikundi na wameungana pamoja.

Jinsi ya kuhakikisha kikundi kinafanya kazi yake

Kikundi kina uongozi ambao umeongoza shughuli zao kwa miaka 17 iliyopita. Kikundi hiki kimesajiliwa rasmi na Idara ya Halmashauri ya Eneo na Msajili Mkuu, ambapo idara hiyo ina majukumu ya kusajili vikundi vya kijamii. Kikundi hiki hukutana kila baada ya wiki mbili ili kuweka mipango, kujadiliana changamoto na kukubaliana ufumbuzi.

Ili kuhakikisha kuna nidhamu na maendeleo, wanachama, pamoja na uongozi wamejiwekea utaratibu wa kimaadili unaoainisha malengo muhimu ili kwamba kuwe na kuheshimiana, kuaminiana, njia za kutatua tofauti na kuweka kuridhika kwa wateja wao kama kipaumbele cha kwanza. Kwa kufanya mikutano, wanabadilishana taarifa, wanatathmini masuala ya ubora na kujadiliana kuhusu fursa mpya za masoko.

Kuimarisha uchakataji wa samaki

Kwa kufanya kazi pamoja, kikundi hiki kimekuwa kikivuka vikwazo vingi ambavyo ni vigumu kwa mtu kuvishinda akiwa peke yake, kwa mfano, kuchakata samaki haraka na kwa namna ya usafi. Kikundi kimeweka utaratibu na wavuvi kuhakikisha kwamba wanapata samaki wenye ubora wa juu kwa ajili ya kuchakata. Hii inafanyika kwa wao kuwapa wavuvi mabonge ya barafu ili kuwahifadhi samaki katika hali ya ubora hadi watakapofkishwa katika eneo la uchakataji. Mara baada ya samaki kufika ufukweni, wanasafirishwa haraka wakiwa katika barafu hadi katika kituo cha uchakataji. Wakifikishwa katika kituo cha uchakataji, samaki wanaachwa ili wakauke kiasi. Ukaushaji wa samaki kwa moshi hufanyika katika wavu wa chuma ulio safi unaowekwa juu ya mkaa katika tanuru lililoimarishwa. Utaratibu huu hufanya bidhaa za samaki zipate rangi nzuri ya kuvutia ya kahawia. Samaki wanapokuwa tayari, huachwa wapoe na kisha kufungashwa katika mifuko ili kutunza ubora na kuwekewa nembo au leboya kikundi. Hii ni aina ya njia rahisi ya kuongeza thamani.

Manufaa ya kufanya kazi pamoja

Kwa kuunganisha nguvu, wanawake wanazalisha bidhaa zenye ubora wa juu zaidi na wanagawana faida. Kwa pamoja wanawake hawa wameweza kupata kile ambacho wasingalikipata kwa kila mmoja kufanya kazi peke yake.

Tazama video

<https://youtu.be/Dj53CORuDis>



©FAO/Yaa Danso



Pitisha simu kwenye
alama hii ili kutazama
video

